BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 27 Septemba, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

10. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Wananchi wanapohitaji kufanya mirathi wanatakiwa waende Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana hata kama wananchi hao wanatoka maeneo ya mbali.

    Kwa nini Kamisheni hii isifungue ofisi zake ndogo ndogo kwa masheha kwa ajili ya kutoa huduma za mirathi.

89. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Serikali ya Awamu ya Nane imeamua kuboresha utendaji wake kuwa wa kisasa zaidi mawizarani katika eneo la fedha kwa kutumia mifumo mbali mbali, hasa ya kielektroniki. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya uelewa wa matumizi ya mifumo hiyo.

    (a) Je, Serikali imechukua juhudi gani kwa watendaji wake kuwapa mafunzo juu ya mifumo hiyo kabla haijaanza kutumika.

    (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaendeleza mafunzo hayo kwa watendaji wengine ili kuwa endelevu zaidi.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

21. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Skuli ya Sekondari ya Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (J.K.U) ni miongoni mwa skuli zinazofanya vizuri hapa Zanzibar. Hali hii inatokana na juhudi kubwa za kuiimarisha kielimu skuli hiyo, zinazofanywa na J.K.U. Hata hivyo, skuli hiyo bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa walimu.

    (a) Je, Wizara yako imejipanga vipi kukabiliana na upungufu wa walimu katika skuli ya J.K.U hapo Mtoni.

    (b) Je, kuna mpango wowote wa kuwatumia walimu bingwa wanaostaaafu japo kwa kuingia nao mkataba, hadi hapo watakapopatikana walimu wa kutosha wenye uwezo mkubwa wa kuwafundisha wanafunzi wa skuli hiyo.

49. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Licha ya jitihada za viongozi wa jimbo kupambana na suala la kuzagaa kwa majaa ndani ya jimbo la Mwanakwerekwe, bado tatizo hili halijapata ufumbuzi.

    Je, ni upi mkakati wa Manispaa ya Magharibi "B" wa kuhakikisha sasa inachukua jitihada za makusudi za kutuondolea majaa kwenye maeneo ya makaazi ya watu ili kuepusha maradhi mbali mbali.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

91. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Katika kukusanya mapato, Serikali inawatumia wadau mbali mbali ambao ni muhimu sana, ikiwa ni pamoja na wakadiriaji na wathamini wa bidhaa mbali mbali. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko yanayotokana na kazi za wathamini na wakadiriaji.

    (a) Je, Serikali kwa sasa inao wathamini na wakadiriaji (Valuers) wangapi wa bidhaa.

    (b) Je, wakadiriaji hawa hutumia mbinu na utaratibu gani kujua thamani halisi ya bidhaa mbali mbali ambazo hununuliwa kutoka nje ya nchi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

83. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Vazi ni sehemu ya utamaduni na utambulisho wa sehemu husika.

    Je, vazi au kivazi kipi hasa ni utambulisho wa Mzanzibari.

**Wizara ya Afya:**

63. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Miongoni mwa huduma zilizo na upekee wa nchi yetu tofauti na nchi nyingi duniani, ni ile sera ya Serikali yetu tokea kumalizika kwa Mapinduzi ya mwaka 1964 ya matibabu yote kuwa ni bure kwa wananchi wote. Aidha, huduma hii pia iliendana na chakula cha wagonjwa kilichotolewa kwa kila mgojwa aliyelazwa katika hospitali za Serikali.

    (a) Kuna mpango gani wa kupatiwa chakula wagonjwa wanaolazwa katika hospitali za Serikali.

(b) Ni kwa nini baadhi ya wagonjwa wanaolazwa katika hospitali hizo huletewa chakula na jamaa zao badala ya chakula hicho kutolewa na Wizara pekee.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

79. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya katika Sekta ya Elimu, ikiwemo kuwapatia zawadi wanafunzi wanaofaulu kwa daraja la kwanza. Hata hivyo, walimu waliofanya kazi nzuri na kusababisha ufaulu huo wanakosa zawadi kama sehemu ya pongezi na motisha itakayowawezesha wazidi kufanya kazi vizuri zaidi.

Je, Serikali haioni haja ya kuwapatia zawadi walimu hao ikiwa kama ni motisha ya kufanya vizuri katika kazi zao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2022/2023.

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**27 Septemba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**